

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA NANE**

**KIKAO CHA NANE**

**22 SEPTEMBER, 2022**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA NANE

**KIKAO CHA NANE – TAREHE 22 SEPTEMBER, 2022**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2022 [*The Written Laws (Financial Provisions) (Amendments) Bill, 2022*].

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2022 [*The Written Laws (Financial Provisions) (Amendments) Bill, 2022*].

### III. MASWALI:

#### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

#### 114. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itakarabati Kituo cha Afya Bungu Wilayani Korogwe.

#### 115. MHESHIMIWA PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (UBUNGO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, nini hatma ya Wananchi wa Ubungo Kisiwani waliofanyiwa tathmini ya kulipwa fidia ili wapishe ujenzi wa mradi wa mabasi yaendayo kasi.

## **WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

### **116. MHESHIMIWA JANETH ELIAS MAHAWANGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni,  
Sanaa na Michezo:-

Je, ni lini Serikali itawekeza katika Sekta ya michezo hasa kwenye timu za Wanawake ili kuibua vipaji kwa Watoto.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **117. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI (NKASI KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na  
Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka usafiri wa majini Ziwa Tanganyika.

### **118. MHESHIMIWA ALLY JUMA MAKOA (KONDOA):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na  
Uchukuzi:-

Je, kuna mpango wowote kubadili mwelekeo wa ujenzi Barabara ya Tanga kupitia Handeni, Kiberashi, Mrijo, Mondo Bicha hadi Kwamtoro.


**119. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO  
MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali haioni ipo haja ya kuufanya Uwanja wa KIA kutumika kuinua kilimo na kuruhusu ndege za mizigo kutua bila kulipa *Landing Fees*.



**WIZARA YA NISHATI:**



**120. MHESHIMIWA REUBEN NHAMANILO  
KWAGILWA (HANDENI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme Mitaa 28 ya Jimbo la Handeni Mjini ambayo bado haijapata umeme.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **121. MHESHIMIWA ERICK JAMES SHIGONGO (BUCHOSA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itawamegea eneo Wakazi wa Kisiwa cha Maisome kutoka Msitu wa Hifadhi ya Maisome.

### **122. MHESHIMIWA NICODEMUS HENRY MAGANGA (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya Askari wa Misitu wanaopiga na kuwanyang'anya mkaa Wananchi wa Mbogwe.

### **123. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-


Je, ni lini Vibali vya Uwindaji vitatolewa.

**WIZARA YA MAJI:**

**124. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Mradi wa Maji wa Halmashauri 28 ambapo Njombe ni mojawapo utaanza kutekelezwa.



**WIZARA YA KILIMO:**

**125. MHESHIMIWA DEUS CLEMENT SANGU (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, nini mpango wa kujenga Skimu ya umwagiliaji Kata ya Kaoze, Kipeta na Kilangawana kwa kutumia Mto Momba Kwela.

**126. MHESHIMIWA ALLY MOHAMED KASSINGE  
(KILWA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Ripoti ya Ukaguzi ya Chama cha Msingi Nanjirinji A itatolewa ili hatua zichukuliwe kwa Wahujumu wa fedha msimu wa 2021/2022.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**127. MHESHIMIWA RAMADHAN SULEIMAN  
RAMADHAN (CHAKECHAKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo kipya cha Polisi katika Wilaya ya Chakechake.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**128. MHESHIMIWA NEEMA GERALD  
MWANDABILA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-



Je, nini mkakati wa Mahakama kutoa hukumu ya pande mbili hasa Mtuhumiwa anaposhinda kesi kuepuka kufungua kesi mpya kulipwa fidia.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**129. MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA (KISESA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni kwa nini kesi 1,097 za kodi zenye thamani ya shilingi Trilioni 360 na Dola za Marekani milioni 181.4 hazijaamuliwa hadi sasa.



**130. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni lini Sheria ya Manunuzi na Ukandarasi kupitia *Public Private Partnership* itaanza kutumika.

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

### 131. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,  
Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itaifanya Elimu ya Sekondari  
kuwa ya lazima.

### 132. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,  
Sayansi na Teknolojia:-

Je, kwa takwimu ni Wahitimu wangapi wa Kada  
ya Ualimu wa masomo ya Sayansi na Hesabu  
hawajaajiriwa tangu Mwaka 2015.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO  
YA MAKAZI:**

**133. MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI  
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi,  
Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Wananchi wa  
Kata ya Majengo—Tunduma waliovunjiwa  
nyumba zao.

**IV. UCHAGUZI WA WABUNGE WA BUNGE LA  
AFRIKA MASHARIKI (EALA):**

**V. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na  
Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria  
Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2022 [*The Written  
Laws (Financial Provisions) (Amendments) Bill, 2022*].

**DODOMA  
22 SEPTEMBER, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**